GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXXI Nam. 7054 **11 Novemba , 2022** **Bei Shs. 2000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti *Hutolewa kila Ijumaa*

Yaliomo.....Uk

Sheria ya Mfuko wa hifadhi ya Jamii Zanzibar Nam.2 ya 2005 kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (Fao la Upotevu wa Ajira)

[Chini ya kifungu cha 44] .....

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la sheria lililotajwa hapo chini limetangazwa katika Gazeti Rasmi hili

Tangazo la Sheria

Nam. 148:-
Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (Fao la Upotevu wa Ajira)

TANGAZO NAM. 148

SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR NAM. 2 YA 2005

KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (FAO LA UPOTEVU WA AJIRA)
[Chini ya kifungu cha 44]

MPANGILIO WA KANUNI

KANUNI	MAELEZO

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1Jina fupi na kuanza kutumika.
2.Ufafanuzi.

Matangazo yaliyohusu mąiti, kuvunjikia kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakla zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

SEHEMU YA PILI
UTARATIBU WA MAOMBI NA MALIPO YA FAO LA UPOTEVU WA AJIRA

3.Kustahili Fao la Upotevu wa Ajira.
4.Utaratibu wa maombi ya Fao la Upotevu wa Ajira.
5.Malipo ya Fao la Upotevu wa Ajira kwa mara ya pili.
6.Njia za kulipa Fao la Upotevu wa Ajira.
7.Kuzuiliwa kwa michango kusubiri mafao ya muda mrefu au malipo mengine.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI MENGINEYO

8.Mamlaka ya Waziri juu ya Fao la Upotevu wa Ajira.
9.Wajibu wa kuwasilisha taarifa zinazohusiana na ajira.
10.Kuendelea na uwanachama na kuchangia.

JADWELI

SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR NAM. 2 YA 2005

KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (FAO LA UPOTEVU WA AJIRA)

[Chini ya kifungu cha 44]

KWA UWEZO niliopewa chini ya kifungu cha 44 vya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar Nam. 2 ya 2005, Mimi, **DKT. SAADA MKUYA SALUM,** Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar natunga Kanuni zifuatazo:

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (Fao la Upotevu wa Ajira), 2022 na zitaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Waziri na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Ufafanuzi

2. Katika Kanuni hizi, isipokuwa itakavyoelezwa vinginevyo.

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar iliyoanzishwa chini ya masharti ya Sheria;

"Fao la Upotevu wa Ajira" maana yake ni kiwango maalum cha fedha taslimu kinacholipwa kwa mwanachama wa Mfuko aliyepoteza ajira kwa mujibu wa masharti yaliyoelezwa katika Sheria na taratibu zilizoelezwa katika kanuni hizi;

"Mafao ya Muda Mrefu" maana yake ni kiinua mgongo, pencheni, mafao ya urithi na mafao ya ulemavu;

"Mwanachama" maana yake ni mwanachama wa Mfuko na haitajumuisha mwanachama wa Mfuko wa Hiari;

"Mfuko" maana yake ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar;

"Mfuko wa Uchangiaji wa Hiari (ZVSSS)" maana yake ni Mfuko wa Hiari ulioanzishwa chini ya masharti ya Sheria;

"Mkurugenzi Mwendeshaji" maana yake ni Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar aliyeteuliwa chini ya chini ya masharti ya Sheria;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Nam. 2 ya 2005;

"Tathmini ya Uhimilivu wa Mfuko" maana yake ni tathmini ya kitaalamu inayopima uwezo wa Mfuko kumudu kuendelea kulipa mafao kwa muda maalumu;

"Waziri" maana yake ni Waziri anaeshughulikia masuala ya fedha.

SEHEMU YA PILI
UTARATIBU WA MAOMBI NA MALIPO YA FAO LA UPOTEVU WA AJIRA

Kustahili Fao la Upotevu wa Ajira

.3.– (1) Kila mwanachama anastahili kulipwa Fao la Upotevu wa Ajira kutoka Mfuko endapo ametimiza masharti yaliyowekwa katika Sheria na taratibu zilizoelezwa katika Kanuni hizi.

(2) Bila ya kuathiri masharti yaliyowekwa katika Sheria, Fao la Upotevu wa Ajira litalipwa kwa mwanachama aliyepoteza ajira mara baada ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi.

(3) Mwanachama ambaye atalipwa Fao la Upotevu wa Ajira kwa mujibu wa masharti ya kanuni ya 6(1)(c) ya Kanuni hizi, atastahili kulipwa fao hili ndani ya vipindi visivyozidi vitatu vya miezi kumi na nane katika mzunguko wa ajira yake.

(4) Mwanachama ambaye ataendelea kukosa ajira ndani kipindi cha miezi ishirini na nne kutoka siku ya mwisho aliyolipwa Fao la Upotevu wa Ajira kwa mujibu wa masharti ya kanuni ya 6(1)(c) ya Kanuni hizi, michango yake itahamishiwa katika Mfuko wa Hiari na atasajiliwa kuwa mwanachama wa Mfuko wa Hiari.

(5) Katika kuzingatia kipindi cha kupoteza ajira kisichopungua miezi sita wakati wa malipo ya Fao la Upotevu wa Ajira, miezi sita itatafsiriwa kuwa mwanachama awe amepoteza ajira ndani ya kipindi cha miezi sita mfululizo katika mwaka unaohusika.

(6) Katika kufanya maamuzi juu ya mwanachama kustahili kulipwa Fao la Upotevu wa Ajira kwasababababu ya kuachishwa kazi kwa makosa ya rushwa, ubadhirifu au kwa sababu ya kushiriki katika shughuli za siasa, Mfuko utazingatia ipasavyo sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia makosa au masuala hayo.

Utaratibu wa maombi ya Fao la Upotevu wa Ajira.

4.– (1) Mwanachama atawasilisha maombi ya Fao la Upotevu wa Ajira kwa kujaza fomu maalum ya maombi kama ilivyoelezwa katika Jadweli la Kanuni hizi.

(2) Mwananachama atawasilisha fomu ya maombi ya Fao la Upotevu wa Ajira iliyojazwa kwa ukamilifu ikiambatana na:

(a) barua binafsi ya maombi ya Fao la Upotevu wa Ajira;

(b) barua ya kusitishwa ajira, kuachishwa kazi au kumalizika muda wa mkataba wa kazi kutoka kwa mwajiri wa mwisho wa mwanachama husika;

(c) uthibitisho kuwa mwanachama hayupo katika ajira yoyote kutoka Kamisheni ya Kazi, Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma Zanzibar na kiapo kutoka Mahakamani;

(d) mkataba wa ajira au kazi uliomalizika ambao Muombaji alikuwa ameajiriwa kupitia Mkataba huo;

(e) taarifa za hesabu yake ya Benki; na

(f) hati nyengine yoyote itakayohitajika na Mfuko.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) na (2) ya kanuni hii, Mkurugenzi Mwendeshaji anaweza kupokea na kukubali hati au ushahidi mwingine wowote unaotilia nguvu maombi ya Fao la Upotevu wa Ajira iwapo ataona inafaa.

(4) Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa kanuni hii, mwombaji wa Fao la Upotevu wa Ajira ambaye alikuwa mtumishi wa umma atawasilisha uthibitisho kuwa hayupo katika ajira yoyote kutoka Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma na mwombaji ambaye alikuwa mfanyakazi katika sekta binafsi atawasilisha uthibitisho kuwa hayupo katika ajira yoyote kutoka Kamisheni ya Kazi Zanzibar.

Malipo ya Fao la Upotevu wa Ajira kwa mara ya pili

5. Mwanachama ambaye ataomba Fao la Upotevu wa Ajira kwa mara ya pili na kuendelea atapaswa kulipwa fao hilo ikiwa amechangia tena katika Mfuko kwa muda usiopungua miezi ishirini na nne kutoka mara ya mwisho alipolipwa Fao la Upotevu wa Ajira.

Njia za kulipa Fao la Upotevu wa Ajira

6.– (1) Mwanachama aliyetimiza masharti yaliyoelezwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi, atalipwa Fao la Upotevu wa Ajira katika moja ya njia zifuatazo:

(a)marejesho ya michango yote kwa mwanachama ambaye amechangia katika Mfuko kwa kipindi cha miezi kumi na nane na kisichozidi miezi thelathini na sita;

(b)marejesho ya michango yote pamoja na faida ya asilimia moja ya jumla ya michango ya mwanachama atakayokuwa nayo kwa mwaka kwa wakati huo kwa mwanachama ambaye amechangia katika Mfuko kwa kipindi cha kuanzia miezi thelathini na sita na kisichozidi miezi sitini na tano; au

(c)malipo ya asilimia ishirini ya jumla ya mishahara ya miezi sita bora kwa mwanachama ambaye amechangia katika Mfuko kwa kipindi kilichofikia zaidi ya miezi sitini na tano.

(2) Mwanachama atalipwa Fao la Upotevu wa Ajira katika njia moja tu miongoni mwa njia tatu zilizoainishwa katika kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii kwa kuzingatia idadi ya miezi ya uchangiaji, na hakuna mwanachama atakayelipwa fao hilo katika njia zaidi ya moja kwa wakati mmoja.

(3) Malipo ya Fao la Upotevu wa Ajira yatalipwa moja kwa moja katika akaunti ya benki ya mwanachama au kwa njia nyengine yoyote ambayo Mkurugenzi Mwendeshaji ataona inafaa.

(4) Mfuko utalipa Fao la Upotevu wa Ajira baada ya mwanachama kukamilisha taratibu za maombi zilizoelezwa katika Kanuni hizi kwa mkupuo.

(5) Mwanachama ambaye atalipwa Fao la Upotevu wa Ajira kwa mujibu wa utaratibu ulioelezwa katika kanuni ndogo ya (1)(c) ya kanuni ya hii, idadi ya miezi ambayo imelipwa Fao la Upotevu wa Ajira itapunguzwa katika jumla au idadi ya miezi ya uchangiaji wakati wa kuhesabu muda wa uchangiaji wakati wa malipo ya mafao ya muda mrefu.

(6) Mfuko unaweza kuanzisha na kulipa Fao la Upotevu wa Ajira katika mfumo mwengine wowote unaokubalika kwa kadri utakavyoona kuwa inafaa kulingana na uwezo wa Mfuko kwa wakati huo baada ya kufanya tathmini ya uhimilivu wa Mfuko.

Kuzuiliwa kwa michango kusubiri mafao ya muda mrefu au malipo mengine.

7. Endapo mwanachama amefanya kazi kwa kipindi fulani amechangia katika Mfuko na akapoteza ajira kwasababu ambazo hawezi kulipwa Fao la Upotevu wa Ajira au hakutimiza masharti ya kulipwa Fao la Upotevu wa Ajira, michango ya mwanachama huyo haitastahiki kurejeshwa na itazuiliwa na Mfuko kusubiri kulipwa mafao ya muda mrefu au malipo mengine atakayostahili kwa mujibu wa Sheria.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI MENGINEYO

Mamlaka ya Waziri juu ya Fao la Upotevu wa Ajira.

8. Waziri, kwa kushauriana na Bodi, anaweza kuongeza au kupunguza viwango vya malipo ya Fao la Upotevu wa Ajira au faida kwa kadri atakavyoona inafaa kwa kuzingatia uwezo wa Mfuko kwa wakati huo na hali halisi ya uhimilivu wa Mfuko kutokana na tathmini za uhimilivu wa Mfuko zinazofanywa kila baada ya kipindi cha miaka mitatu.

Wajibu wakuwasilisha taarifa zinazohusiana na ajira

9.–(1) Katika kufanikisha ulipaji wa Fao la Upotevu wa Ajira, kila mwajiri atakuwa na wajibu wa kuwasilisha taarifa za ajira za kila mfanyakazi wakati atakapomwajiri na mkataba wa mfanyakazi husika utakapomalizika au atakapomwachisha kazi.

(2) Mwajiri atawasilisha taarifa za ajira katika Mfuko au Kamisheni ya Kazi Zanzibar ndani ya kipindi kisichozidi siku saba baada ya kumuajiri mfanyakazi husika, kumalizika mkataba wa ajira au kumuachisha kazi mfanyakazi wake.

Kuendelea na uwanachama na kuchangia

10.Endapo mwanachama amelipwa Fao la Upotevu wa Ajira na uwanachama wake kusita kwasababu ya kupoteza ajira, ataendelea na uanachama wake na kuchangia wakati wowote atakapopata ajira nyengine.

JADWELI

FOMU YA MAOMBI YA FAO LA UPOTEVU WA AJIRA

[Chini ya kanuni ya 4(1)]

SSF14

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR
S.L.P 2716 ZANZIBAR
FOMU YA MAOMBI YA FAO LA UPOTEVU WA AJIRA

(Tafadhali soma kwa uangalifu kabla ya kujaza fomu hii na tumia herufi kubwa tu). Fomu hii ijazwe mbele ya Afisa wa ZSSF.

MAELEZO

1. Fomu hii itatolewa bila ya malipo.
2. Fomu hii ni lazima ijazwe na mwanachama ambaye anaomba fao la ukosefu wa ajira.
3. Fomu hii ijazwe baada ya mwanachama kuthibitishwa kuwa ana sifa za kupata Fao la Upotevu wa Ajira.
4. Mwombaji ni lazima aambatanishe barua ya maombi ya mafao ya upotevu wa ajira ya mwanachama, barua ya kusitishwa ajira au kuachishwa kazi au kumalizika muda wa mkataba wa kazi kutoka kwa mwajiri wa mwisho wa mwanachama uthibitisho kutoka Kamisheni ya Kazi, Ofisi ya Kuu ya Utumishi wa Umma Zanzibar na kiapo kutoka Mahakamani kuwa mwanachama hana ajira.
5. Fomu hii ijazwe nakala mbili.

KWA MATUMIZI YA OFISI:

Imepokelewa na kuangaliwa na……..

Saini ……..Tarehe……

……

MUHURI WA ZSSF

SEHEMU "A"
MAELEZO YA MWOMBAJI

1.Jina kamili la Mwombaji _____

2.Nambari ya Uanachama wa ZSSF……

3.Anuani ya Mwombaji……

4.Umri……
5.Uraia ……

6.Nambari na Aina ya Kitambulisho.....

7.Nambari ya simu ya mkononi.....

8.Barua pepe ya Mwombaji.....

9.Tarehe ya uliyojiunga na ZSSF.....

10.Tarehe ya kumaliza mkataba wa kazi au kuachishwa kazi.....

11.Naomba kulipwa mafao ya upotevu wa ajira ninayostahiki kwasababu;

a.Nimeachishwa kazi mnamo tarehe.....

b.Nimemaliza mkataba wa kazi mnamo tarehe.....

SEHEMU "B"
MALIPO YA MAFAO YA UPOTEVU WA AJIRA.

Tamko la mwombaji kulipwa mafao ya upotevu wa ajira moja kwa moja katika hesabu yake ya benki.

Natamka kuwa nimekubali kulipwa mafao ya upotevu wa ajira kupitia hesabu yangu ya benki iliyoainishwa hapa chini:

Jina la Benki: _____
Tawi la Benki: _____
Nambari ya Hesabu: _____
Jina la mwenye Hesabu ya Benki: _____

Naambatanisha pamoja na vielelezo vinavyohusika kwa ajili ya Fao la Upotevu wa Ajira.

Nathibitisha kwamba maelezo yote niliyoyatoa katika fomu hii ni ya kweli na yananifunga kisheria.

Saini ya Mwombaji: _____ Tarehe: _____.

IMETIWA saini tarehe 10, Oktoba 2022.

.....
(DKT. SAADA MKUYA SALUM)
WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO
ZANZIBAR.

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI - ZANZIBAR 2022